

KURUDISHA UASILI WA ARDHI KUPITIA MRADI WA ReDEAL

MASWALA YA KUZUNGUMZIA

MAARIFA

1. Uharibifu wa ardhi ni nini, na unaweza kusababishwa na niini?
2. Ni kwa namna gani mfumo wa ikolojia bionuai unachangia ustahimili? Ni kwa namna gani viumbeuanai kwenye mfumo-ikolojia huchangia uimara wake?

UFHAMU

3. Nini tofauti kati ya mbinu ya usimamizi wa ardhi ya chini-juu na juu-chini?
4. Kwa nini wakulima na wanasayansi wana mitizamo tofauti juu ya uharibifu wa ardhi na kurudisha uasili wake?
5. Kwa nini ni muhimu sana kwa ReDEAL kufanya kazi na wakulima wazawa kuweza kutafuta suluhisho la uharibifu wa ardhi?

MATUMIZI

6. Ni maswali gani ambayo ungewauliza wakulima katika maeneo ya utafiti nchini Kenya kuhusu vipaumbele vya yale ambayo wangependa kuyafahamu kuhusu matumizi ya ardhi zao?

UCHANGANUZI

7. Jopo la ReDEAL linajumuisha wanaikolojia, wataalamu wa elimukilimo, wanasayansi wa udongo, wanaanthropolojia, wanasayansi ya jamii, mwanasayansi wa mazingira na mwanajiojografia. Unafikiri kila aina ya mtaalamu anachangia vipi kufikia malengo ya mradi?

TATHIMINI

8. Maeneo mengi sana ulimwenguni, wanasayansi wa viumbe vya majini wanafanya kazi katika sekta ya uvuvi kutafuta njia endelevu za kusimamia mfugo wa samaki na kuhifadhi mfumo-ikolojia bahari. Ni mafunzo gani kutoka katika mradi wa ReDEAL unafikiri yanaweza kutumika kwa muktadha huu?
9. Idadi ya watu barani Afrika inatarajwa kuongezeka karibu mara mbili ifikapo mwaka wa 2050. Je, unafikiri hili linaweza kuathiri vipi jamii za vijijini ambazo mradi wa ReDEAL unafanya nao kazi?

Kwenda kwenye ukurasa wa tovuti Futurum ya Mariana na Joseph kwa tafsiri ya lugha ya kiingereza na uhuishaji kuhusu tafiti zao:
www.futurumcareers.com/bringing-life-back-to-kenyas-grasslands

SHUGHULI UNAZOWEZA KUFANYA UKIWA NYUMBANI AU DARASANI

Katika miaka ya 1930, athari za miongo kadhaa ya matumizi mabaya ya ardhi yalisababisha kupotea rutuba kwa Nyanda Kuu za Kusini mwa Marekani. Kipindi hiki kilijulikana kama Bakuli la Vumbi (Dust Bowl) kwa kuwa kilisababisha vimbunga vikubwa vya vumbi na kuharibika kwa mazao ndani ya eneo lote. Watu wengi sana walifariki na hii ilichangia madhara ya mporomoko mkubwa wa uchumi, kufanya maelfu ya familia kuwa masikini. Soma zaidi hapa:
www.history.com/topics/great-depression/dust-bowl.

Fikiria kwamba umerudishwa nyuma kiwakati hadi mwanzoni mwa karne ya ishirini kwenye harakati za kubadilisha historia na kuepusha Bakuli la Vumbi. Ni namna gani ungetumia mafunzo uliyojifunza nyakati za sasa, kama ulivyojifunza kutokana na mradi wa ReDEAL, kuweza kushughulikia visababishi vya Bakuli la Vumbi?

Kwa kuzingatia zana na njia zinazotumiwa na mradi wa ReDEAL kusaidia kuharakisha kurudisha uasili wa ardhi nchini Kenya. Hizi zinajumuisha tafiti za kisayansi, kutumia maarifa ya wazawa, uwezeshaji wa chini-juu na kuhusisha jamii.

Katika majibu yako, elezea sababu za kibiolojia, kijamii na za kiuchumi ambazo zilizopelekea kutokea kwa Bakuli la Vumbi.

- Kufanya kilimo cha kina kama vile kulima kwenda chini zaidi
- Kuondoa nyasi za asili za prairie ambazo zilisaidia kuzuia uharibifu wa ardhi
- Kuongezeka kwa wakulima wapya wasiokuwa na uzoefu, waliotokana na sheria ya kitaifa iliyosaidia kutanua kilimo.

Imani isiyo na misingi lakini iliyosambaa eneo kubwa kuwa kulima katika Uwanda Mkubwa kutafanya hilo eneo kuwa na hali ya hewa ya mvua za juu la wastani

- Kuongezeka kwa mahitaji ya ngano kama vile kutoka Ulaya kipindi cha Vita ya kwanza ya Dunia

Buni pendekezo la kuwashawishi wakulima, wasimamizi wa ardhi na serikali kubadili matumizi ya ardhi na usimamizi wake katika maeneo ya Nyanda Kuu za Kusini. Ni kwa namna gani utahamasisha ushiriki wa jamii? Ni kwa namna gani utawezesha mbinu ya chini-juu badala ya juu-chini?

TAARIFA ZAIDI

-Habari zaidi kuhusu mradi wa ReDEAL zinaweza kupatikana kwenye tovuti:

wp.lancs.ac.uk/restoringafricangrazing

-Tazama video hii kutoka ReDEAL, ambayo inamahojiano na wakulima wa Kenya kuhusu namna walnavyofanya usimamizi wa ardhi yao: www.youtube.com/watch?v=lnVGWz9nVFI&t=571

-Makala hii fupi kutoka kwa mtengenezaji wa filamu Amy Browne inachunguza namna ambayo wakulima wa Australia wanavyokabiliana na uharibifu wa ardhi na kukuza kilimo kinachojizalisha: www.youtube.com/watch?v=6vQW8TL_KLc

-Makala hii kutoka Umoja wa Mataifa inaelezea uharibifu wa ardhi na kurudisha katika uasili wake ardhi kote barani Afrika: www.un.org/africarenewal/magazine/december-2021/we-need-moonshotfrica%E2%80%99s-land-restoration-movement